

Aelezea wasiwasi juu ya fedha

ASILIMIA 70 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Serikali, haziwafikii walengwa, kwa mujibu wa naibu wa Spika wa Bunge, Bw Farah Maalim.

Akizungumza na wanahabari mjini Naivasha katika warsha ya kutengeneza bajeti, Bw Maalim alieleza wasiwasi wake juu ya hasara ya mabilioni ya fedha kila mwaka kwa sababu ya ufisadi katika mashirika mbalimbali ya Serikali.

“Rushwa katika idara mbalimbali za Serikali ni kizuizi cha maendeleo ya nchi na kunahitajika hatua za dharura ili Wakenya wasiendelee kuteseka,” alisema. Bw Maalim wakati huo huo alitetea matumizi ya (CDF) akisema kwamba, karibu asilimia 75 ya fedha zilizodhamiriwa kuwafikia wananchi mashinani, zilitumika kwa miradi ya manufaa.

Mbunge huyo wa Lagdera alionekana kujibu ripoti iliyotolewa na chama cha Walipa Ushuru (NTA), iliyoeleza kuwa zaidi ya Sh400 milioni za hazina ya CDF zilifujwa katika maeneo 28 ya ubunge.

-Na JOYCE KIMANI